

Maswali

1. Mbona Yesu aliamrisha wanafunzi wake watoke kwa mashua?
2. Yesu alikuwa anafanya nini walipoondoka kwa mashua?
3. Mbona wanafunzi walikuwa na shida ya kuendesha mashua?
4. Waliona nini ikitembea juu ya maji?
5. Walifikiria ilikuwa nini?
6. Alikuwa nani?
7. Petro alitaka kufanya nini?
8. Nini ilifanyika alipoacha kumuangalia Yesu?
9. Yesu alifanya nini kumwokoza Petro?
10. Upepo na mawimbi yalifanya nini?
11. Masomo gani tunajifunza hapa?

Majibu

1. Kwa sababu walitaka kumfanya Mfalme.
2. Alienda mlimani kuomba.
3. Upepo uliwapinga na bahari ilikuwa chafu.
4. Mtu.
5. Walifikiria ilikuwa pepo.
6. Alikuwa Yesu anawakujia.
7. Alitaka kutembea juu ya maji afike alikokuwa Yesu.
8. Alianza kuzama.
9. Alinyosha mkono wake akamshika.
10. Zilitulia papo hapo.
11. Tunajifunza kwamba Yesu hutulinda na kutuombea; kwamba ni la muhimu kukaa na wanaomtumikia Mungu; kwamba tukiacha kanisa tutapotelea duniani; lakini tukiendelea kumtafuta Yesu kama mwokozi na tumtumikie, tutashinda ulimwengu. Hata tukiogopa na kukata tamaa, tukimuangalia na kumtegemea Yesu, atatusaidia. Siku moja Yesu atarudi na tutakuwa naye kwa Ufalme wa Mungu wa amani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



37 Petro atembea juu ya maji

Marejeo

Mathayo 14:22—23

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba ni lazima tuweke imani yetu kwa Yesu.

Maneno maalum

1. Baada ya 5000 + mashua + Yesu anaachwa nyuma
2. Upepo mkali + giza + Yesu aliona
3. Mtu juu ya maji + ogopa + ona Yesu
4. Petro + kuja + enda kwa Yesu
5. Angalia chini + zama + niokoe
6. Imani ndogo + nyanyua + kwa mashua
7. Dhoruba ikaisha + sitaajabu + Kapernaumu
8. Masumbuko ya dunia + jaribu kufika kwa Ufalme
9. Kaa kwa mashua + na Yesu
10. Amini Yesu + Soma Biblia + kutana pamoja
11. Yesu anaungana nasi + pumzika + dunia istarehe

37.1 Yesu alikuwa amelisha wanaume 5000 pamoja na wake na familia zao kutoka kwa mikate tano na samaki wawili wadogo. Watu walisitaajabia huo uwezo na wakataka kumfanya mfalme papo hapo. Kuzuia hili jambo, kwa haraka Yesu aliambia wanafunzi wake waingia kwa mashua na waende Kapernaumu hali anawaaga watu waende. Yeye akaenda vilimani kuomba.

37.2 Wanafunzi walipata shida ya kusafiri kwenda Kapernaumu kwa sababu upepo mkali ulipiga mashua yao. Baada ya mwendo mfupi, giza iliingia. Huko kwa vilima alikokuwa Yesu akiomba aliona vile wanafunzi walikuwa wakipata shida wakijaribu kuendesha mashua kwa bahari iliyochafuka.



37.3 Walipokuwa wakiendesha mashua waliona mtu akitembea juu ya maji. Walistaajabu na kuogopa wakifikiria kwamba ni pepo. Walilia kwa hofu. Huyo mtu alipokuja karibu waliona kwamba ni Yesu na akawaita na kusema, “Msiogope, ni mimi.”

37.4 Petro alimuita na kusema, “Bwana, kama kweli ni wewe, nataka nikuje huko ulioko.” Yesu alimuita amuendee. Petro alitoka mashuani na kukanyaga kwa bahari iliyokuwa imechafuka. Alimkazia Yesu macho na kuenda. Alitembea juu ya maji! Chini ya miguu yake maji yalimpiga piga akikaribia Yesu.

37.5 Alipoangalia chini miguuni mwake kwa maji, uoga ulimshika. Upepo ulivuma saidi na mawimbi yakapanda juu. Petro akaanza kupungukiwa na imani. Akaanza kuzama baharini. Akamlilia Yesu na kusema, “Bwana niokoe.”

37.6 Yesu alinyosha mkono wake akamnyanyua. Akamwambia, “Petro mbona imani ndogo, mbona unashaka?” Pamoja walishikana mikono na kwenda kwa mashua kulikokuwa na wanafunzi wengine. Walikaribiswa kwa mashua.

37.7 Mara Yesu na Petro walipoganyaga kwa mashua upepo ulitulia. Wanafunzi walishangaa sana, wakamsujudia Yesu na kusema kweli yeye ni Mwana wa Mungu. Kulipokucha walikundua kwamba wamefika Kapernaumu bila shida.

37.8 Sisi wafuasi wa Yesu tuko kama wanafunzi wa Yesu kwa mashua. Vile Biblia inasema ametutuma juu ya bahari, pahali pengi penye dunia ya machafuko mengi isiyo na amani. Wanafunzi walitaka wafike Kapernaumu kwenye “kijiji cha utulifu.” Hata nasi tunajaribu tufike kwa Ufalme wa Mungu kwenye tutapumzika. Yesu anatuomba kwa Mungu na anatuona vile tunamenyana na shida za maisha.

37.9 Ni muhimu sisi wafuasi wa Yesu tukae pamoja kwa mashua. Tukiondoka inamaanisha tutapotelea ulimwenguni. Tufanye kazi pamoja kwa nia moja ya Ufalme. Wakati mwingine shida zinatuzonga mpaka tunakata tamaa. Wakati huo lazima tukumbuke kwamba Yesu yuko karibu na anatuangalia. Hata bahari ikichafuka kwa sababu aliishinda ulimwengu haitamshinda.

37.10 Tukiwa na imani kwa Yesu, nasi tutashinda ulimwengu lakini kukuwa na imani hii inatulazimu tukaze macho yetu kwa Yesu, tukisoma Biblia na kukutana pamoja tukimkumbuka kila juma. Tunapofanya hivi hata tukiwa pekee yetu ulimwenguni tusiogope kuzama ama tukipungukiwa na imani, tujue kwamba Yesu atanyosha mkono wake atushike.

37.11 Siku moja Yesu atajumuika nasi pamoja na watakatifu waliokuweco wote. Vile bahari ilitulia, hata dunia hii na shida zote zitaisha tupumzike na kufarijika. Ukweli ni kwamba dunia yote itajua yeye ni mwana wa Mungu.